# Haki ya Mafarisayo

# Haki ya Waamini



PASTOR JAMES KALEKWA

# HAKI YA MAFARISAYO,
# HAKI YA WAAMINI

James Kalekwa

## Yaliyomo kitabuni:


Salamu za Mama Mchungaji JK. ............ 4

Timiza Wokovu wako! .............................. 6

Kuhusu haki ya Mafarisayo. ....................12

Farisayo ni nani? .........................................16

Ni watu wa kuyachunguza Maandiko 23

Ni watoaji wa sadaka na dhabihu mbalimbali .................................................. 25

Ni washuhudiaji na wavunaji wa nafsi. ........................................................................ 28

Ni waombaji wanaojidhabihu. ...............31

Ni watu wa  matendo ya huruma. ........33

Kuhusu Mwandishi: ................................ 35

Kuhusu New Vine Church: .................... 36

Mawasiliano na Mwandishi: ..................37

# Salamu za Mama Mchungaji JK.

Juni 20, Mungu alitupa zawadi ya maisha ya mtumishi wake Pastor JK, mtu wa juhudi nyingi katika Kristo na maarifa ya kimungu. Kwa muda ambao nimekuwa naye kwenye maisha, nimemtambua kama mtu anayempenda Mungu kiasi cha mimi kukosa neno la kuelezea. Huyu ni mtu aliuzwa kwa Mungu na utumishi!

Amewekeza muda mwingi kuandika mfululizo wa vitabu hivi vya kielektroniki ili avitoe bila malipo kama sehemu yake ya ujenzi wa mwili wa Kristo… kwa niaba yake, ninaomba ukipokee kwa kuthamini dhabihu! Ninakuombea ya kwamba maisha yako yanageuzwa kwa kitabu hiki kimoja tu kwa jina la Yesu Kristo.

Pili, ninaomba uwasambazie kitabu hiki watu wengi zaidi ili maono ya kuujaza ulimwengu kwa maarifa ya utukufu wa Mungu kama maji yaifunikavyo bahari yatimilizwe.

Na hatimaye, kwa kuthamini zawadi ya mtu huyu wa Mungu, muombee, mwandikie ujumbe wa kumsalimu na kumsherehekea ukimweleza namna gani umesadika na utumishi wake – itafaa sana.

Heri ya siku ya kuzaliwa mume wangu mpenzi. Heri ya kuzaliwa Pastor JK – zawadi ya mbingu kwenye kizazi chetu!

Frida James Kalekwa (Mama mchungaji JK)

Mke wa mwandishi

Juni, 2025

Dodoma, Tanzania

# Timiza Wokovu wako!

Wafilipi 2:12-13 SUV *"Basi, wapendwa wangu, kama vile mlivyotii sikuzote, si wakati mimi nilipokuwapo tu, bali sasa zaidi sana mimi nisipokuwapo,* ***utimizeni wokovu wenu wenyewe kwa kuogopa na kutetemeka.*** *Kwa maana ndiye Mungu atendaye kazi ndani yenu, kutaka kwenu na kutenda kwenu, kwa kulitimiza kusudi lake jema."*

Fundisho la Biblia ni kwamba wokovu hupatikana kwa neema kwa njia ya imani ambayo hiyo ni kipawa/zawadi ya Mungu kutoka kwa Mungu. Pia, ni fundisho la Biblia kwamba mtu aliyeamini anapaswa

kuenenda sawasawa na kuamini kwake. Kunapaswa kuwe na uhusiano baina ya kuamini na kuenenda. Na hapo ndipo huja fundisho la mwenendo wa mwamini karibia kwenye nyaraka zote za mtume Pauolo.

Tazama maneno haya, *"utimizeni wokovu wenu kwa kuogopa na kutetemeka"* hapa kuna namna na kuna mkao *"posture"* kuuhusu wokovu. Wazo kuu ni kama vile mtu uliyekabidhiwa mbegu mikononi mwako. Mazingira yote yamewekwa tayari kukupa ushirikiano na kukuzalia matunda. Ni wajibu wako kufanya kitu na mbegu iliyowekwa mikononi mwako ili uone

matunda husika. Hilo ndilo wazo nyuma ya kuutimiza wokovu wako!

Wokovu umeletwa lakini umewekewa namna ya kuutimiza ambayo ni ka kuogopa (reverence) na kutetemeka! Hii siyo hofu kama ile ya kutishwa au kudhania linaweza kukupata jambo baya, bali ni hofu inayozaliwa kutokea kwenye upendo na umakinifu kwa sababu ya kiwango cha kimahusiano ulichonacho na mtu husika… kwenye andiko hili mahusiano yako na Mungu.

Si tu kwamba tumeambiwa tubebe wajibu binafsi kuhusiana na kuifanyia kazi mbegu ya wokovu… kuutimiza wokovu bali pia

tumeelekezwa namna ya kuutimiza wokovu! Si vyovyote vile.

Umewahi kusikia kuhusu *hofu ya Mungu?* Hii ni hofu takatifu. Si kwa sababu anatutisha au atatuua, bali ni kwa sababu ya uzuri na utakatifu wake.

Hebu nikutazamishe walau Maandiko pendekezwa kuhusu hofu, kuogopa na kutetemeka kama jambo chanya.

Isaya 6:5, *"Ndipo niliposema,* **Ole wangu! *Kwa maana nimepotea; kwa sababu mimi ni mtu mwenye midomo michafu, nami ninakaa kati ya watu wenye midomo***

***michafu; na macho yangu yamemwona Mfalme, BWANA wa majeshi.****"*

Luka 5:8, *"Simoni Petro alipoona hayo, alianguka magotini pa Yesu, akisema,* ***Ondoka kwangu, kwa kuwa mimi ni mtu mwenye dhambi, Bwana."***

**Luka 24:32**, *"Wakaambiana,* ***Je! Mioyo yetu haikuwaka ndani yetu hapo alipokuwa akisema nasi njiani****, na kutufunulia maandiko?"*

Biblia imejaa mifano mingi ya namna hii ya kwamba kila mara uungu unafunua sehemu yake, hofu hutanda… kwa sababu ni jambo la thamani na umaalum! Sasa, ndicho

kinachozungumzwa kuhusiana na kuufanyia kazi wokovu wetu.

Hali zote mbili, yaani hofu na kutetemeka, zinaonyesha ni kwa kiwango gani, uangalifu kiasi gani, kuthamini, kuupenda na kuuthamini wokovu. Mara zote kuogopa na kutetemeka ni hali zinazotokea pale unapoliekeka jambo kubwa ambalo ukiharibu kidogo tu linagharimu maisha yako yote kwa namna fulani hivyo linadai uangalifu mkubwa sana na nidhamu kubwa sana, na sasa kiwango hiki ndivyo mwamini anapaswa kuuchukua wokovu na kuuona hivyo na si chini ya hapo.

# Kuhusu haki ya Mafarisayo.

Mathayo 5:20 SUV *"Maana nawaambia ya kwamba*, ***Haki yenu isipozidi hiyo haki ya waandishi na Mafarisayo,*** *hamtaingia kamwe katika ufalme wa mbinguni."*

Moja ya Maandiko ambayo nimepigana nayo mueleka ili kuelewa hasa muktadha, historia na kisha tafsiri yake hili mojawapo! Inakuwaje haki ya wanafunzi izidiwe na haki ya Mfarisayo ambao Bwana Yesu kutwa kucha amekuwa akiwakosoa katika mafundisho yake? Kwa haki ya Mafarisayo ndiyo ikoje? Nilihangaika sana!

Bwana Yesu anatumia maneno haya kuwaarifu wanafunzi wake kuwa wakatenge muda wao na kuwasoma mafarisayo na wajue haki zao na anasema wakishakuzijua hizo haki wao wanapaswa kwenda mbele na kuwazidi mafarisayo na kinyume cha hapo wakatakuwa hawana sehemu katika ufalme wa mbinguni. Yaani, ufalme wa Mungu unataka haki zaidi kuliko kile wanachojishughulisha nacho Mafarisayo.

Mara kadhaa watu wengi kwenye ukristo tumeonyesha uelewa hasi kuwahusu Mafarisayo; ama hatuwaelewi au tumepokea habari mbaya kutokea kwa

waliotutafsiria na kutufundisha. Mafarisayo wametajwa kama watu ambao wanapingana na Injili ya Yesu Kristo!

Sasa hapa kwa Mara ya kwanza Yesu Kristo analinganisha haki yao na anaitaja kama rejea kwa ajili ya kujifunza kwa wanafunzi wake; hii inasema kwamba kumbe kuna mambo mafarisayo walifanya yalikua yanafaa kuigwa, kujifunza na kuendelezwa. Isipokuwa ukifuatilia kwa umakini, Bwana Yesu katika huduma yake, kila mara alipowakosoa Mafarisayo ilikuwa hasa ni kwenye swala la nia ya ndani au msukumo nyuma ya kutenda kwao.

Ninajaribu kudhani ya kwamba inawezekana mimi na baadhi ya wenzangu tungefeli huu mtihani wa kuiga haki ya Mafarisayo. Tungesema, *"Aaah kumbe kipimio ni Mafarisayo... basi mtihani ni mwepesi sana huu, nitapiga mia kwa mia!"*

Kabla haujauingia mtego niliosema ningeweza kuingia, hebu tuwe na wakati kuwatambua watu hawa ambao Yesu anasema wakawe rejea kwa wanafunzi wake kwenye swala la kuwa na haki na kuingia mbinguni.

## Farisayo ni nani?

a) Farisayo ni mtu aliyeyatoa maisha yake yote kujifunza, kuelewa, kuitii, kutunza torati/sheria ya Bwana (tunaposema torati hapa kwa lugha nyepesi ni Maandiko Matakatifu) kwenye ngazi binafsi na kwenye ngazi ya kundi.

Luka 18:21, *"Akasema, Hayo yote* ***nimeyashika tangu utoto wangu.****"*

Umewahi kushuhudia mashindano ya hadhara ya kitaifa na kimataifa ambapo watu wa imai fulani huonyesha ni kwa namna gani wamehifadhi (wamekariri kwa kichwa) kitabu mwongozp cha

imani? Hivi unajua imegharimu muda kiasi gani kufanya hivyo?

Sasa, huo ni mfano mdogo wa maana halisi ya Farisayo! Ninaomba ujue ya kwamba Farisayo hakuwa mtu mchovu, mjinga au wa kuchukuliwa kwa wepesi. Alikuwa ni moja ya wajuzi wa Maandiko ya wakati huo!

b) Farisayo ni mtu aliyeyatoa maisha yake yote kuishika torati kwa kuiishi na kuilinda wakati wote.

Ezra 7:10, *"Kwa maana huyo Ezra alikuwa* ***ameuelekeza moyo wake kuitafuta sheria***

***ya BWANA, na kuitenda, na kufundisha*** *maagizo na hukumu katika Israeli."*

Wafilipi 3:5, *"Nalitahiriwa siku ya nane, ni mtu wa taifa la Israeli, wa kabila ya Benyamini, Mwebrania wa Waebrania,* ***kwa habari ya kuishika torati, ni Farisayo.****"*

Uelewa nyuma ya mtindo huu wa maisha ni kwamba torati ilikuwa inaendelea kufifia kwa kadiri mud unavyoendelea mbele. Kuna vizazi vinakuja ambavyo havitamjua Mungu; tamaduni za dunia zilianza kuwaingilia na hivyo, utamaduni wao hususani upande wa imani ungefifia na kujifia kifo asilia!

,farisayo waliyatoa maisha yao kuwa ndiyo "benki" ya torati – kwa ufahamu na kwa matendo, mwenendo na maisha yao kwa ujumla!

c) Farisayo ni mtu aliyejitoa kuitetea torati wakati wote na mahali popote pale.

Wafilipi 3:6, *"**kwa habari ya juhudi, mwenye kuliudhi Kanisa**, kwa habari ya haki ipatikanayo kwa sheria sikuwa na hatia."*

Mafarisayo walikuwa radhi kupingana hadharani kwa hoja; kwa fujo na kwa hila na mbinu za kisiasa na mtu yeyote ambaye

anaonekana ni tishio kwenye uwepo wa sheria ya Mungu kwa watu wa Israeli. Unaelewa ya kwamba hivyo ndivyo alivyokuwa Mtume Paulo hapo awali!

Kwa sababu hizi utaona mafarisayo kama Yusufu wa Arimathaya pamoja na Nikodemo walimwendea Yesu nyakati za usiku kwa sababu taratibu za kundi la mafarisayo hazikuruhusu mtu awe na ushirika na nje ya kuitii torati; na walitambua athari za kupatikana kwenye shida hiyo.

Tukirudi kwenye mtiririko wetu Yesu anazungumza kuhusu kuingia kwenye ufalme wa Mungu na hapa niruhusu

nikutazamishe pande hizi mbili ambazo ni ufalme wa Mungu ujao lakini pia ufalme wa Mungu uliopo hapa duniani sasa.

Luka 11:2, “Ufalme wako uje, [Mapenzi yako yatimizwe, hapa duniani kama huko mbinguni.]”

Je, tuombapo hivyo huwa tunaomba kuhusu ufalme wa Mungu ujao baada ya Yesu kuja mara ya pili; au huwa tunaomba ufalme wa Mungu uliopo sasa uliotuijilia kwa ujio wa kwanza wa Yesu na kazi yake na msalaba na ufufuko?

Kimsingi, halipaswi kuwa swala la ama ujao au uliopo bali linapaswa kuwa swala la

ufalme wa milele… Maana yake hata sasa upo! Kwa hiyo, hii inaweza kumaanisha, wanafunzi wakipima chini ya kiwango cha haki ya Mafarisayo wanapoteza sehemu yao kiutendaji katika ufalme wa Mungu kuanzia sasa kwenye maisha haya!

Tupate safari sasa ya kuona ni mambo gani mafarisayo waliyatenda kiasi ambacho Bwana Yesu anawataja kama rejea ya kujifunzia. Yafuatayo ni mambo waliyoyatenda mafarisayo;

## Ni watu wa kuyachunguza Maandiko

Mafarisayo wameshavuka hatua ya kusoma Maandiko (torati/sheria), wako mbele sana kiasi cha kufanya uchunguzi, kuyatafiti na kuyachunguza Maandiko ili kujua uhalisia na ukweli wa kile kilichoandikwa; na ajabu ni kwamba wanafanya hivi maisha yao yote!

Yohana 5:39 SUV *"**Mwayachunguza maandiko,** kwa sababu mnadhani kwamba ninyi mna uzima wa milele ndani yake; na hayo ndiyo yanayonishuhudia."*

Kumbuka muda wote tulikotokea. Bwana Yesu anakemea nia/msukumo wa ndani. Hata hivyo hapingi kitendo kinachofanywa.

Yesu mwenyewe anatambua kuwa hawa mafarisayo kwenye eneo la kuchunguza maandiko sio wa kawaida. Ni jambo moja tu wamekosa ni kujua anayezungumziwa ni Yesu. Mwamini anayetaka kuwa kwenye kiwango cha utakatifu ni kwamba anapaswa kuwa zaidi ya mafarisayo linapokuja swala la yeye na kusoma Maandiko Matakatifu; inagharimu kuyachunguza Maandiko ili kuwa mtakatifu. Huwezi kuchunguza Maandiko, huna sehemu hai katika ufalme wa Mungu!

Utaongozwa kwa namna gani? Utaisikiaje sauti ya Mungu? Utayaishije maisha kwa ujumla? Utaombaje?

Ukikosa Maandiko Matakatifu kwenye ufalme huu, umekosa kila kitu!

## Ni watoaji wa sadaka na dhabihu mbalimbali

Mathayo 23:23 SUV *"Ole wenu waandishi na Mafarisayo, wanafiki! Kwa kuwa mnalipa zaka za mnanaa na bizari na jira, lakini mmeacha mambo makuu ya sheria, yaani, adili, na rehema, na imani; hayo imewapasa kuyafanya, wala yale mengine msiyaache."*

Kumbuka hili muda wote: Bwana Yesu anathamini na kukubaliana na kitendo. Anarekebisha nia ya moyo ya ndani.

Mafarisayo wanatoa zaka kwenye kila kitu kiasi kwamba hata kwenye mambo madogo kama viungo vya chakula! Zaka ya mnanaa, bizari na jira. Na walitenda hivyo ili wapate kuhesabiwa haki!

Wakati upande wa pili damu ya Yesu imekwisha gharamikia swala la haki. Je, si zaidi kwa aliyekwisha pata haki? Mwamini ambaye anateseka bado kwenye eneo la utoaji anatenda chini ya matarajio ya utakatifu kwenye ufalme huu. Huwa ninawaambia mahangaiko waliyonayo

wengi kwenye eneo la utoaji hususani wa sadaka kama vile ya fungu la kumi, huwa ni tangazo la hadhara juu ya shida inayoendelea kwenye moyo/nia ambayo hupelekea tafsiri iliyopotoka kimaandiko.

Bwana Yesu anatuma ujumbe kuwa mtakatifu/mwamini anapaswa kutoa na anatarajiwa kutenda hivyo bila ya kuchunguzwa, yaani kwa hiyari yake mwenyewe kabisa na hii ndiyo itaamua na kuzungumza kuhusu kiwango cha utakatifu kwenye maisha yake.

Mathayo 6:2 SUV *"Basi wewe utoapo sadaka, usipige panda mbele yako, kama*

*wanafiki wafanyavyo katika masinagogi na njiani, ili watukuzwe na watu."*

Swala la utoaji kwa mtakatifu si swala la *"iwapo utatoa/ikiwa utatoa"* bali limo kwenye kundi la *"wakati unatoa iweje.,."*

## Ni washuhudiaji na wavunaji wa nafsi.

Mathayo 23:15 SUV *"Ole wenu waandishi na Mafarisayo, wanafiki! Kwa kuwa mnazunguka katika bahari na nchi kavu ili kumfanya mtu mmoja kuwa mwongofu; na akiisha kufanyika, mnamfanya kuwa*

*mwana wa jehanum mara mbili zaidi kuliko ninyi wenyewe."*

Mafarisayo wanatumia gharama kubwa kwa ajili ya kuhakikisha nafsi ya mtu mmoja tu inaokoka. Wanazunguka katika bahari na nchi kavu; Tafsiri zingine husema wanavuka (kama vile kuvuka mipaka kwenda upande wa pili wa eneo la kijiografia).

Hii inatuma ujumbe mzito kwa mwamini anayetaka kufikia kiwango cha utakatifu kuwa anapaswa kutumia na kulipia gharama kubwa zaidi ya mafarisayo kwa ajili ya kushuhudia wokovu wa mtu mmoja, mwamini asiyejali kuhusu wokovu

kuelekea mwanadamu mwingine anatuma ujumbe kuwa hana uelewa wowote kuhusu utakatifu.

Kumbuka Bwana Yesu anapongeza kitendo cha uvunaji wa nafsi na kukemea nia na namna yao katika uvunaji wa nafsi!

Haki ya mwamini inapaswa kuzidi haki ya mafarisayo!

## Ni waombaji wanaojidhabihu.

Mathayo 23:14 SUV" [Ole wenu waandishi na Mafarisayo, wanafiki! Kwa kuwa mnakula nyumba za wajane, na kwa unafiki **mnasali sala ndefu**; kwa hiyo mtapata hukumu iliyo kubwa zaidi.]"

Marko 2:18 SUV *"Nao wanafunzi wake Yohana na Mafarisayo* ***walikuwa wakifunga****; basi walikuja, wakamwambia, Kwani wanafunzi wa Yohana na wanafunzi wa Mafarisayo hufunga, bali wanafunzi wako hawafungi?"*

Mafarisayo walikuwa sio wanaomba tu bali kuna kina cha maombi walifika kiasi

ambacho kimetajwa na Yesu kuwa wanafanya sala ndefu, yaani wanaomba muda mrefu na wakati Yesu anashughulika nao hakemei swala la sala ndefu bali nia nyuma ya sala nefu! Hivyo ni ujumbe kuwa sala ndefu ndiyo namna ya kuomba na imeruhusiwa kabisa. Mwamini anatarajiwa kuwa mteja wa maombi ya muda mrefu, kiwango cha maombi ya mwamini anayetazamia kuwa mtakatifu ni maombi yenye kina cha muda mrefu na sio maombi ya sekunde kadhaa.

Halafu kuna nyongeza kuhusu maombi yao. Yalihusisha na swala la kufunga. Hiyo ndiyo ilikuwa haki ya mafarisayo!

## Ni watu wa  matendo ya huruma.

Mathayo 23:14 SUV *"[Ole wenu waandishi na Mafarisayo, wanafiki! Kwa kuwa mnakula nyumba za wajane, na kwa unafiki mnasali sala ndefu; kwa hiyo mtapata hukumu iliyo kubwa zaidi.]"*

Mafarisayo wanatenga muda wanatoka kwenda kuwatembelea wajane na wanafanya hivi kwa watu wenye uhitaji kama njia ya kutimiliza matendo ya huruma kwao. Kuwa mwamini mtakatifu inadai kutoa mali na vitu vya thamani kuyaelekea maisha ya wahitaji ili yawe bora zaidi.

**Kuhusu Mwandishi:**

Mwandishi wa kitabu hiki, James Kalekwa, ni mfuasi wa Yesu Kristo; mtoto wa kiroho wa Mchungaji Goodluck na Ziada Kyara; Mume mpenzi wa Frida, baba anayewajibika wa Joshua-Vision, Charis "Tai", Victor na Priscilla na Butogwa; na anafurahia kuwa mchungaji mkazi wa kanisa la New Vine jijini Dodoma.

Mchungaji James ameitwa *"Kuujaza ulimwengu kwa maarifa ya utukufu wa Mungu kama maji yaifunikavyo bahari."* [Habakuki 2:14]

**Kuhusu New Vine Church:**
Kanisa la New Vine limebeba utume wa kuinua kizazi cha kiungu kitakacholeta mguso chanya kwenye kila nyanja ya maisha kwenye jamii, taifa na mataifa. (Mathayo 5:13-14/Yoeli 2:2-11)

Makao makuu ya kanisa (Gloryland) yako Mwanza chini ya mwangalizi ambaye pia ni muasisi, Mchungaji Goodluck & Mama Ziada Kyara.

Kufahamu zaidi kuhusu kanisa hili kwa ujumla tembelea: https://www.newvinechurch.or.tz

**Mawasiliano na Mwandishi:**

Iwapo unahitaji kupata mafundisho zaidi ya maandishi na audios kutoka kwa mwandishi wa Kitabu hiki, Mchungaji James Kalekwa. Unaweza kufanya hivyo kupitia channel ya telegram: https://t.me/nvcdodoma AU fungua app ya telegram kisha tafuta @nvcdodoma

Unaweza pia kumfuatilia mwandishi kupitia mitandao ya kijamii:

Facebook: Pastor James Kalekwa

Instagram: @pastorjameskalekwa

Youtube: Pastor James Kalekwa

Twitter: @MchungajiJK

Iwapo una ushuhuda, unahitaji ushauri na msaada wa kichungaji unaweza kuwasiliana naye moja kwa moja kupitia +255-754-917-764 (Kupiga simu, SMS na WhatsApp)

NEW VINE CHURCH | Dodoma



New Vine Church limebeba utume wa kuinua kizazi cha kiungu kitacholeta mguso chanya kwenye kila nyanja ya maisha kwenye jamii, taifa na mataifa *(Mathayo 5:13 -14/Yoeli 2:2 - 11).*

Makao makuu ya kanisa (Gloryland) yako Mwanza chini ya mwangalizi ambaye pia ni muasisi, Mchungaji Goodluck & Mama Ziada Kyara.

Kufahamu zaidi kuhusu kanisa hili kwa ujumla tembelea: https://www.newvinechurch.or.tz



**Mahali tulipo:** Swaswa mkabala na geti la Waziri Mkuu, Dodoma mjini.

## Ratiba za Ibada

**Alhamisi** Saa 11:15 jioni - saa 12:15 jioni
**Jumapili** Saa 3:00 asubuhi - saa 6:30 mchana

nvc_dodoma +255 754 917 764

# KUHUSU MWANDISHI



James Kalekwa ni amemwamini Yesu kuwa BWANA na Mwokozi wa maisha yake. Ni mtoto wa kiroho wa Mchungaji Goodluck na Ziada Kyara; ni mume mpenzi wa Frida; baba anayewajibika kwa Joshua-Vision, Charis "Tai", Victor ,Priscilla na Butogwa. Ni mchungaji wa New Vine Church - Dodoma


pastorjameskalekwa
+255 754 917 764
pastorjameskalekwa
pastorjameskalekwa
pastorjameskalekwa
pastorjameskalekwa
MchungajiJK
+255 754 917 764
jameskalekwa.com